Atakayemuua aliyechukua ahadi ya kulindwa, hatonusa harufu ya pepo, na hakika hurufu yake hupatikana kuanzia mwendo wa miaka arobaini

Imepokewa Kutoka kwa Abdillah Ibn Amri -Radhi za Allah ziwe juu yao wawili- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-amesema: "Atakayemuua aliyechukua ahadi ya kulindwa, hatonusa harufu ya pepo, na hakika hurufu yake hupatikana kuanzia mwendo wa miaka arobaini".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Anabainisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- tahadhari kubwa kwa atakayemuuwa aliyechukua ahadi ya kulindwa -Naye ni kafiri aliyeingia katika mji wa kiislamu kwa ahadi na amani- kuwa hatonusa harufu ya Pepo, na hakika harufu yake huwa kuanzia umbali wa mwendo wa miaka arobaini.

https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/64637

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

لجنة الدعوة الإلكترونية
EDC E-Da'wah Committee